download more resources here: https://kcserevision.com

## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Ingawa matokeo ya jumla ya somo la Kiswahili katika mwaka wa 2020 yameimarika, utendaji wa asilimia kubwa ya wanafunzi ungali hafifu. Hili linadhihirika kwa matokeo ya karatasi ya pili, ambayo yalishuka japo kwa kiwango hafifu. Idadi ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu umeimarika kutoka **115,319** mwaka wa 2019 hadi **168,582** mwaka wa 2020. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka minane (2013 hadi 2020).

https://kcserevision.com/membership.join/

***Jedwali 10: Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili (2013 – 2020)***

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2013 | 1 | 445,555 | 40 | 18.46 | 5.44 |
| | 2 | | 80 | 29.92 | 12.68 |
| | 3 | | 80 | 34.82 | 14.92 |
| | Jumla | | 200 | 83.19 | 29.77 |
| 2014 | 1 | 482,122 | 40 | 20.17 | 5.26 |
| | 2 | | 80 | 32.27 | 12.60 |
| | 3 | | 80 | 42.93 | 15.81 |
| | Jumla | | 200 | 95.36 | 29.88 |
| 2015 | 1 | 5211,59 | 40 | 20.86 | 5.19 |
| | 2 | | 80 | 36.12 | 13.50 |
| | 3 | | 80 | 38.80 | 15.38 |
| | Jumla | | 200 | 95.76 | 31.02 |
| 2016 | 1 | 571,176 | 40 | 18.23 | 5.53 |
| | 2 | | 80 | 34.11 | 13.83 |
| | 3 | | 80 | 25.67 | 12.87 |
| | Jumla | | 200 | 77.97 | 29.07 |
| 2017 | 1 | 610,392 | 40 | 18.84 | 5.23 |
| | 2 | | 80 | 25.45 | 11.79 |
| | 3 | | 80 | 25.15 | 13.42 |
| | Jumla | | 200 | 69.43 | 27.49 |
| 2018 | 1 | 659,465 | 40 | 16.98 | 4.82 |
| | 2 | | 80 | 27.22 | 10.88 |
| | 3 | | 80 | 22.20 | 11.95 |
| | Jumla | | 200 | 66.40 | 24.76 |
| 2019 | 1 | 694,982 | 40 | 19.88 | 5.43 |
| | 2 | | 80 | 36.50 | 12.64 |
| | 3 | | 80 | 21.08 | 12.64 |
| | Jumla | | 200 | 77.46 | 28.03 |
| 2020 | 1 | 743,395 | 40 | 20.19 | 5.28 |
| | 2 | | 80 | 34.99 | 12.81 |
| | 3 | | 80 | 25.88 | 16.00 |
| | Jumla | | 200 | 81.05 | 31.28 |

download more resources here: https://kcserevision.com

download more resources here: https://kcserevision.com

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

(i) Utendaji wa watahiniwa katika utungaji umeimarika. Haya yanadhihirishwa na kupanda kwa alama wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) kutoka **19.88** mwaka 2019 hadi **20.19** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **36/40**. Ni watahiniwa **watatu** tu ambao walipata alama hii. Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(64,786)** ni **23/40.** Alama hii ni sawa na ya mwaka wa 2019. Hali kadhalika, idadi ya watahiniwa ambao walipata asilimia sabini **(70%- 28/40)** ilipanda kutoka **18,718** mwaka 2019 **(2.69%)** hadi **29,597 (3.94%)** mwaka huu .

(ii) Hata hivyo, uchanganuzi umedhihirisha kwamba bado kuna idadi ya wanafunzi **(1,453)** waliopata alama moja **(1).** Hakika wanafunzi **9874(1.31%)** walipata baina ya alama **1** na **5.** Pia karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(5.28 )** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida **(15.00).** Hali hii inaweza kuhusishwa na watahini kuwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

(iii) Alama ya wastani ya karatasi ya pili **(102/2)** imeshuka kwa pointi **1.51** kutoka **36.50** mwaka 2019 hadi **34.99** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **76/80**. Alama hii ni sawa na ile iliyotuzwa mwaka wa 2019. Ni wanafunzi **wanane** tu ambao walipata alama hii. Wanafunzi **377** walipata baina ya alama **70/80** na **76/80**. Idadi hii iliongezeka ikilinganishwa na mwaka wa 2019 ambapo idadi ya wanafunzi waliopata alama baina ya **70/80** na **76/80** ilikuwa **180.** Aidha alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(21,623)** ni **33/80.** Hali kadhalika, idadi ya wanafunzi waliopata asilimia sabini **(70%- 56/80)** katika karatasi hii ilipanda kutoka **8,140 (1.17%)** mwaka wa 2019 hadi **41,136 (5.47%** mwaka huu. Aidha, imebainika kwamba karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ilikuwa **12.81** kinyume na **12.64,** ya mwaka wa 2019.

(iv) Hata hivyo, bado kuna asilimia ya wanafunzi ambao walipata alama za chini. Kwa mfano, wanafunzi **5,979,** walipata baina ya alama **1** na alama **5** ikilinganishwa na watahiniwa **3,616** waliopata baina ya alama **1** na alama **5** mnamo mwaka wa 2019. Hali kadhalika, ruwaza za matokeo zinaonyesha kuwa matokeo ya karatasi hii yamekuwa yakiyumba tangu mwaka wa 2009. Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi (10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta tatu sufuri** (**14.30** ) mwaka 2012. Mwaka 2013 ilipanda kwa kiasi kidogo mno, mwaka 2014 kwa **2.35,** na mwaka 2015 kwa takriban alama **4**. Mwaka 2016 alama ilishuka kwa takriban alama **2**, Mwaka 2017 alama hii ilishuka kwa zaidi ya alama **8**. Mwaka 2018 alama wastani ilipanda kwa takriban alama **2** mwaka wa 2019 ilipanda kwa alama **9.28** na mwaka huu kushuka kwa alama **1.51**.

(v) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2020 yameimarika kwa takriban alama **4.80** kutoka alama wastani **21.08** mwaka 2019 hadi **25.88** mwaka huu. Alama ya juu zaidi iliytuzwa ni **76/80.** Ni watahiniwa **7** ndio waliopata alama hii. Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi **(30, 890)** ni alama **01/80 (4.11%).** Hii inamanisha kwamba wanafunzi hawa walipata sufuri katika kila swali. Aidha wanafunzi **86,175** (11**. 59%)** walipata baina ya alama **1** na **5** jambo linalodokeza kwamba wanafunzi hawa hawakusoma vitabu vya fasihi**.** Hali kadhalika, ni wanafunzi **4,443** ambao walipata asilimia sabini **(70%- 56/80)** katika karatasi hii. Hii ni asilimia **( 0.59%)** ya watahiniwa **742,995** ambao walifanya karatasi hii. Hili ni dhihirisho la kuimarika kwa matokeo ikilinganishwa na wanafunzi **646** waliopata alama hizi mnamo mwaka wa 2019.

download more resources here: https://kcserevision.com

download more resources here: https://kcserevision.com

(vi) Alama wastani ya somo la Kiswahili kwa jumla imepanda kwa alama **3.59** kutoka **77.46** mwaka 2019 hadi **81.05** mwaka huu.

(vii) Kadhalika asilimia ya watahiniwa wanaopata gredi A na A- ilipanda, japo haijafikia kiwango cha kuridhisha.

(viii) Alama wastani ya somo hili bado haijafikia kiwango cha kuridhisha cha **(100/200).**

### 3.2.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

#### 3.2.2.1 INSHA (102/1)

***Jedwali 11: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2013– 2020***

| Mwaka | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** | **2018** | **2019** | **2020** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 18.46 | 20.17 | 20.86 | 18.23 | 18.84 | 16.98 | 19.88 | 20.19 |
| Alama ya Tenganisho | 5.44 | 5.26 | 5.19 | 5.53 | 5.23 | 4.82 | 5.43 | 5.28 |

https://kcserevision.com/membership/join/

Jedwali hili linaonyesha kwamba, kwa kipindi cha miaka minne (2017-2020), utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umekuwa ukiyumba. Tathmini ya kazi halisi za watahiniwa imebainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haimudu kujieleza kwa lugha iliyokomaa. Ni wazi kwamba idadi kubwa ya watahiniwa haikuweza kukuza mada inavyostahili. Aidha, asilimia kubwa ya watahiniwa ilipata chini ya nusu ya alama zilizotengewa karatasi hii **(1/40- 19/40)**. Tathmini ya kazi za watahiniwa pia imeonyesha kwamba watahiniwa wengi hawamudu tungo za kiuamilifu. Baadhi ya watahiniwa wanazingatia muundo wa tungo hizi bila kushughulikia maudhui ya swali kikamilifu. Kwa mfano, ingawa swali la kwanza liliwahitaji watahiniwa kuonyesha umuhimu wa vyuo vya kiufundi, wengi walipotoka, walijadili mikakati ambayo serikali na washikadau wanapaswa kuzingatia ili kuviboresha vyuo hivi. Baadhi ya watahiniwa hawakumudu kuandika tungo zao wakizingatia muundo wa Ripoti. Kadhalika watahiniwa hawamudu maswali yanayoshughulikia masuala mtambuko. Asilimia kubwa ya watahiniwa haikuweza kuonyesha umuhimu wa kuwepo kwa magazeti katika maktaba ya shule. Wengi wa watahiniwa walijadili ama umuhimu wa maktaba kwa jumla au manufaa ya maktaba kwa jamii pana. Hii ni ishara kwamba wanafunzi wengi, ama wamekosa ubunifu, au hawana mazoea ya kusoma kwa kina na kwa mapana. Kadhalika imebainika kwamba swali linalohusu methali halipendelewi na wanafunzi wengi. Idadi ya watahiniwa walioteua swali lililohusiana na methali ilikuwa chini. Baadhi ya watahiniwa walioteua swali hili walitatizika katika kung'amua maana na matumzi ya methali husika.

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**1. Lazima**

> Wewe ni katibu wa jopokazi ambalo limeteuliwa kuchunguza sababu za wanafunzi wa shule za upili kupuuza masomo ya kiufundi. Andika ripoti ya uchunguzi huo huku ukitoa mapendekezo.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika Ripoti kuhusu sababu za wanafunzi wa shule za upili kupuuza masomo ya kiufundi.

Tungo za watahiniwa zilidhihirisha kiwango cha chini cha ubunifu. Wengi hawakuweza kukuza mada kikamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

download more resources here: https://kcserevision.com

download more resources here: https://kcserevision.com

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawatilii maanani usomaji wa mapana, hivyo hawadiriki kushughulikia masuala mtambuko ipasavyo katika tungo zao.

**Ushauri kwa walimu**

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, Kenya (KICD).

**Mapendekezo**

(i) Walimu waendelee kuwashirikisha wanafunzi katika mazoezi zaidi katika uandishi wa kazi za kiuamilifu na tungo za kiubunifu.

(ii) Walimu watilie maanani matumizi ya silabasi ya K.I.C.D ili kuelekeza ufundishaji wao. Nyenzo nyinginezo kama vile mwongozo unaotolewa na Baraza la Mitihani kuhusu mada na stadi zinazotahiniwa, pamoja na vitabu vya Fasihi vinavyotahiniwa, zitumiwe kujalizana na silabasi ya KICD.

(iii) Wanafunzi wahamasishwe kuhusu manufaa ya kuboresha stadi ya kusoma hasa kusoma kwa mapana, na kwa kina. Kusoma huku kutapalilia ubunifu wao. Pia kutawawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala ibuka na mtambuko iwapo yatatahiniwa.

### 3.2.2.2 LUGHA (102/2)

**Jedwali 12**: ***Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2013 hadi 2020***

| Mwaka | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Alama ya Wastani** | 29.92 | 32.27 | 36.12 | 34.11 | 25.45 | 27.22 | 36.50 | 34.99 |
| **Alama ya Tenganisho** | 12.68 | 12.60 | 13.50 | 13.83 | 13.42 | 10.88 | 12.64 | 12.81 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameshuka kutoka **36.50** mwaka wa 2019 hadi **34.99** mwaka huu.

Swali la kwanza liliwatatiza baadhi ya watahiniwa. Swali hili liliwahitaji watahiniwa kusoma kifungu cha Ufahamu kisha kujibu maswali. Baadhi ya watahiniwa hawakumudu maswali yaliyowahitaji kutumia ujuzi wao kupata majibu. Haya ni maswali yanayolenga kukuza stadi za kiwango cha juu cha utambuzi kama vile uchanganuzi, usanisi na tathmini.

Swali la pili nalo liliwahitaji watahiniwa kusoma kifungu kisha kutoa muhtasari wa kifungu hicho kwa kurejelea masuala mbalimbali katika kifungu kwa mujibu wa maswali yaliyoulizwa. Baadhi ya watahiniwa hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo; walinakili yale yaliyokuwa katika kifungu, na kuishia kupoteza alama kwa kuzidisha idadi ya maneno, wengine walifupisha japo hawakuzingatia swali, hivyo kukosa alama kwa kuwa hawakujadili hoja zilizohitajika.

Swali la tatu lilikuwa la Matumizi ya lugha.

Swali la nne lilitahini Isimujamii. Sajili iliyotathminiwa ilikuwa ya Hotuba za Kisiasa. Japo watahiniwa wengi walielewa sajili hii, hawakumudu kulishughulikia swali hili kwa kina kwa kupungukiwa na hoja. Vilevile wengi wa watahiniwa walikuwa na makosa ya sarufi na hijai.

Tutachanganua swali la tatu.

download more resources here: https://kcserevision.com

**3. MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

(i) Kipasuo ghuna cha midomoni, irabu ya chini, kati, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya juu mbele

(ii) Nazali ya ufizi, kipasuo ghuna cha kaakaa laini, irabu ya juu, nyuma, irabu ya nyuma wastani

(b) Bainisha silabi zinazowekwa shadda katika maneno yafuatayo: (alama 1)

(i) waliotusifia
(ii) sherehekea

(c) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1)
Nyua walizojenga hapa zimesaidia kukabiliana na wahalifu hao.

(d) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya udogo. (alama 1)
Mbuzi huyo wake ana ngozi laini.

(e) Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na kivumishi kimilikishi. (alama 1)

(f) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo.

(i) Maafisa hao walipewa uhamisho. Maafisa wenginehawakupewa uhamisho. (Unganisha kuunda sentensi ambatano.) (alama 2)

(ii) Hadithi hiyo <u>ilitungwa</u> vizuri <u>ikawavutia</u> wengi. (Badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kuwa nomino.) (alama 2

(iii) Tunda halitaoshwa vyema. Tunda halitalika. (Unganisha kuwa sentensi moja kwa kutumia 'po'.) (alama 2)

(iv) Kengewa alitoa ahadi. Wengi waliiamini ahadi hiyo. (Unganisha kuwa sentensi moja inayoanza kwa: Ahadi.) (alama 2)

(g) Tunga sentensi ya masharti inayoonyesha kwamba kitendo kilifanikiwa kutokana na kufanikiwa kwa kingine. (alama 2)

(h) Tunga sentensi yenye kishazi kirejeshi ambacho ni kielezi. (alama 2)

(i) Ainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

<u>Mwenyewe</u> <u>hakuwa</u> <u>amekupa</u> ruhusa kuitumia.

(j) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 2)
Mwanangu akasema Neema huku amemkazia macho huoni unamtia mwenzako wasiwasi

https://kcserevision.com/membership-join/

download more resources here: https://kcserevision.com

(k) Andika maneno yenye mofimu zifuatazo: (alama 2)

(i) Umoja (ngeli ya U-I), mzizi, kiishio
(ii) Kikanushi, kiambishi ngeli (KI-VI umoja), mzizi, kauli tendeka, kiishio

(l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 2)
K N ( N + R H ) + K T( T + E)

(m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kukanusha. (alama 1)
Ngoma hizo zilihifadhiwa ili ziuzwe mjini.

(n) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali ya mazoea. (alama 2)
Bili atawashauri vijana kuhusu umuhimu wa michezo.

(o) Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Alimfanya Tindi **anywe** pombe ikamfanya **alewe**.

(p) Tunga sentensi ukitumia mzizi, -ingine kumaanisha "baadhi ya". (alama 2)

(q) Hewala ni kwa kukubaliana na jambo, ........................ ni kwa kutaka kitu kinusurike, na ........................ ni kwa aliyefanya vyema katika jambo. (alama 1)

(r) Zito ni kwa jepesi, ........................ ni kwa choyo, na ................. ni kwa kali. (alama 1)

(s) Andika visawe vya kauli zilizopigiwa mstari. (alama 2)

Musei **alikumbwa** na matatizo mengi lakini **hakukata tamaa**.

(t) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana **mbili** za neno: **zima.** (alama 2)

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi. Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi na za matumizi ya lugha kujibu maswali aliyopewa. Imebainika kwamba utendaji wa wanafunzi katika dhana za kimsingi za lugha kama vile uakifishaji, aina za maneno, nyakati na hali, kuandika katika umoja na wingi, na mnyambuliko wa vitenzi, unaendelea kuwa hafifu. Hali kadhalika, tatizo hili lilichangia katika watahiniwa wengi kupoteza alama katika maswali ya Ufahamu, Ufupisho na Isimujamii. Hili ni kutokana na watahiniwa hawa kuwa na makosa ya sarufi na hijai.

**Mapendekezo**

(i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara wakizingatia vipengele vyote vya kisarufi.

(ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba stadi zote hutathminiwa hasa maswali ya stadi za juu kama vile matumizi/utekelezaji na usanisi. Wasijikite tu katika maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye muktadha uliotolewa au kukariri kutoka kumbukizi zao.

download more resources here: https://kcserevision.com

https://kcserevision.com/membership-join/

download more resources here: https://kcserevision.com

(iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya Ufahamu na Muhtasari mara kwa mara huku wakihimizwa kuzingatia mtiririko ufaao ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

(iv) Walimu wasisitize vipengele vyote vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

(v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe. Mathalan mwalimu anaweza kutumia Fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na masomo mengine hivyo kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.

(vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

(vii) Masuala yote katika silabasi yazingatiwe.

https://kcserevision.com/membership-join/

### 3.2.2.3 FASIHI (102/3)

**Jedwali 13**: ***Matokeo ya Karatasi ya tatu (102/3) ya miaka 2013 hadi 2020***

| Mwaka | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 34.82 | 42.93 | 38.80 | 25.67 | 25.15 | 22.20 | 21.08 | 25.88 |
| Alama ya Tenganisho | 14.92 | 15.81 | 15.38 | 12.87 | 13.42 | 11.95 | 12.64 | 16.00 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii uliimarika japo kwa kiwango cha chini. Idadi kubwa ( **30,890**) ya watahiniwa ilipata alama **1/80.** Hali kadhalika, karatasi za watahiniwa zimebainisha kwamba changamoto kuu inayoukumba utendaji wa wanafunzi katika Fasihi ni ama kutozingatia vipengele muhimu katika kuvisoma vitabu viteule au kutovisoma vitabu hivyo. Ithibati ya haya ni kutoweza kutambua mhusika katika muktadha uliotolewa pamoja na kuchanganywa kwa wahusika; mtahiniwa akajadili sifa za mhusika mwingine badala za yule aliyelengwa na swali. Vilevile, watahiniwa kutomudu kutambua muktadha wa dondoo lililotahiniwa. Kadhalika, kazi za watahiniwa zilibainisha kutomudu maswali ambayo yalimhitaji mtahiniwa kujadili umuhimu wa vipengele vya kiploti kama vile mandhari katika kuvijenga vipengele vingine vya kazi husika kama vile wahusika na maudhui. Yaelekea kwamba ujifunzaji wa Fasihi Simulizi ni hafifu. Wengi wa watahiniwa hawakumudu kujibu maswali yaliyowahitaji kupata majibu kutoka kwenye tungo lililotahiniwa. Watahiniwa hawa hawakumudu kujibu maswali yaliyolenga kukuza stadi za kiwango cha juu cha utambuzi kama vile uchanganuzi, usanisi na tathmini hasa lile lilitowahitaji kufafanua mambo ambayo wanaweza kutenda ili kufanikisha shughuli za utambaji.

Hali kadhalika, tathmini ya karatasi halisi za watahiniwa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa, hata wale wanaopata alama za juu zaidi katika karatasi hii, bado haimudu kuwasilisha hoja kwa njia komavu. Kazi za watahiniwa zimepwezwa na makosa mengi ya kisarufi, kimuundo na hijai. Kadhalika, pameibuka mtindo wa kuwasilisha hoja kwa ufupi mno, bila kuzitolea mifano na maelezo kutoka matini husika ya kifasihi. Hili linawafanya watahiniwa wengi kupoteza alama. Vile vile maswali ya ushairi yangali yanaepukwa na watahiniwa wengi. Hata wale wanaodiriki kuyashughulikia, wanaambulia alama za chini. Imebainika kwamba baadhi ya masuala ya kimsingi ya ushairi hayafunzwi, hivyo yanapotokea katika mtihani watahiniwa wengi hupoteza alama kwa kutoweza kung'amua masuala husika. Hawamudu kutumia ujuzi wa dhana husika kujibia maswali.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.

download more resources here: https://kcserevision.com

download more resources here: https://kcserevision.com

## SEHEMU A: HADITHI FUPI

**A. Chokocho Na D. Kayanda:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

**1. Lazima**

*D. Kayanda:* "Mwalimu Mstaafu"

(a) "Naomba radhi *mfawidhi* ... lakini nadhani ni jambo la busara kutokitia mchanga kitumbua..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)

(iii) Kwa kurejelea hadithi hii jadili kwa kutoa hoja **kumi** namna mhusika Jairo alivyokitia kitumbua mchanga. (alama 10)

(b) Bainisha vipengele vya kimtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 4)

"Alijaaliwa mvi nyeupe zilizojianika kwenye kichwa chake kidogo kilichosimama *jadidi* kwenye shingo yake nyembamba. Alijaaliwa mvi kwa vile zilikuja mapema wakati akiwa bado ana umri wa miaka thelathini. Watu wakasema hekima hiyo *kutabasuri* huko. Kwa hiyo, hakujisumbua kujipaka rangi nyeusi kuung'ang'ania ujana uliotishia kumwondoka mapema ... mvi zimemkaa kwa haiba kama theluji..."

https://kcserevision.com/membership-form/

Hili lilikuwa swali la kimuktadha ambalo lilimhitaji mtahiniwa kuwa ameisoma hadithi teule kutoka Diwani ya *Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine* na kuelewa ploti ili kubainisha matukio katika hadithi na hivyo basi kung'amua wahusika na matendo yao pamoja na toni ya dondoo husika. Swali hili pia lilihitaji mtahiniwa kuonyesha mwingiliano uliopo kati ya vipengele vya kazi ya kifasihi, hasa vile vya kimtindo katika kuboresha kazi ya kifasihi.

Hata hivyo, uchanganuzi wa utendaji wa watahiniwa katika swali hili, na hata katika maswali mengine ulidhihirisha kwamba wengi wa watahiniwa hawasomi vitabu vya fasihi kwa kina. Watahiniwa hawakuweza kuliweka dondoo katika muktadha. Pia, hawakuweza kutambua toni ya dondoo husika. Kadhalika, wanafunzi wengi hawazielewi istilahi za kimsingi za uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walishindwa kuelewa dhana ya **mahitaji ya kiarudhi** katika swali lilowahitaji kuchanganua mbinu zinazotumiwa na mtunzi wa shairi katika kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika mojawapo wa mashairi yaliyotahiniwa.

**Mapendekezo**

(i) Walimu wawaongoze wanafunzi kuvisoma na kuvichambua vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:

a) Dhamira na maudhui

b) Fani, kama vile:

- Mandhari- Maana na umuhimu wayo
- Ploti- vipengele kama vile mbinu rejeshi, elekezi na sadfa, na umuhimu wavyo
- Usimulizi- nafsi na wakati katika usimulizi
- Wahusika- Sifa na umuhimu wao katika kujenga kazi za kifasihi

download more resources here: https://kcserevision.com

download more resources here: https://kcserevision.com

- Muundo- urudiaji, usambamba….
- Mtindo, kama vile taswira, kinaya n.k

(ii) Wanafunzi wahimizwe kusoma na kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

(iii) Wanafunzi wawekewe misingi bora katika Fasihi Simulizi tangu kidato cha kwanza na kuongozwa kujiimarisha katika mada zote za fasihi simulizi kulingana na upeo uliopendekezwa na mtaala wa Shule za Upili.

(iv) Walimu wawaelekeze wanafunzi wao kutambua na kutumia istilahi muhimu za ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya ushairi.

(v) Mbinu za kuchanganua ushairi zifunzwe katika upana na kina kulingana na kiwango hiki.

(vi) Wanafunzi wakumbushwe kwamba vipengele vya kazi ya kifasihi ni vile vile. Kwa mfano; taharuki na toni huweza kuchanganuliwa katika Ushairi, na vilevile katika tamthilia na tungo za kinathari, kama vile riwaya.

https://kcserevision.com/membership-join/

**Hitimisho**

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba japo utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa jumla umeimarika mwaka huu, matokeo ya karatasi ya Pili yalishuka japo kwa kiwango hafifu. Asilimia wastani ya watahiniwa **(50.27%)** ilimudu kupata tuzo ya wastani ya somo hili ambalo lilikuwa **81.05**. Vilevile ni dhahiri kwamba matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa jumla bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha.

Inatumainiwa kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa. Kadhalika ni muhimu kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuendelea kuimarisha matokeo ya somo hili. Hali kadhalika, ipo haja ya kuandaa warsha na makongamano ili kufanikisha kujadiliwa kwa mada na stadi ambazo zinaelekea kuwatatiza zaidi walimu na wanafunzi.

download more resources here: https://kcserevision.com